**TAARIFA FUPI YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHE. PROF. MAKAME MBARAWA (MB), KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI TAREHE 23 MACHI 2017**

Leo tarehe 23 Machi 2017, Shirika la Hali ya Hewa Duniani (World Meteorological Organization - WMO) pamoja na wanachama wake 191 wa Shirika hili kutoka kote Ulimwenguni wanaungana na Jumuiya ya kimataifa kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani. Siku hii ni kumbukumbu ya kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano wa kuanzishwa kwa WMO uliosainiwa mnamo tarehe 23 Machi, 1950 na hatimaye WMO kuzaliwa rasmi mwaka 1951. Kwa upande wa Tanzania, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilianzishwa mnamo Disemba, 1999 baada ya Serikali kuchukua uamuzi mahsusi wa kuboresha utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa sekta mbali mbali muhimu chini ya sheria ya Wakala wa Serikali No. 30 ya 1997. Kabla ya kuanzishwa TMA huduma hizi zilikuwa zikitolewa na iliyokuwa Idara Kuu ya Hali ya Hewa (DoM) chini ya iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Hivyo ni kwa muktadha huu kuwa kila mwaka tarehe kama hii, Tanzania kama Mwanachama hai wa WMO husherehekea Siku ya Hali ya Hewa Duniani na kuonesha dhamira yetu kama nchi katika kuendeleza huduma za hali ya hewa na matumizi yake kwa jamii.

Katika kusherehekea Siku ya Hali ya Hewa Duniani ni desturi kuwa na kaulimbiu ya maadhimisho inayohusisha hali ya hewa na maisha ya kila siku ya jamii, hivyo kwa mwaka huu kaulimbiu ya maadhimisho inahusiana na namna mawingu

yanavyotumika kutabiri hali ya hewa na athari zake katika hali ya hewa ya sehemu husika, yaani “**Tuyaelewe mawingu na umuhimu wake.** Kaulimbiu hii inaakisi umuhimu wa kuongeza uelewa wa mawingu ili kujua zaidi mchango wake katika mzunguko wa maji kati ya nchi kavu, baharini na angani na uhusiano wake na hali ya hewa ya muda mfupi na mrefu. Kama inavyojulikana kuwa mawingu yana umuhimu mkubwa sana katika mifumo ya hali ya hewa ya dunia na hivyo elimu juu ya tabia ya mawingu itasaidia katika kutabiri hali ya hewa na kutambua mabadiliko ya tabia nchi kwa wakati ujao. Wahenga huwa wanasema, *Dalili ya Mvua ni Mawingu*.

Nichukue fursa hii kupongeza mikakati kabambe na mipango ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ya kuendeleza sayansi ya mawingu na uhusiano wake katika utabiri wa hali ya hewa, na kwa kuhuisha Atlasi ya Kimataifa ya Mawingu (International Cloud Atlas). Atlasi hii mpya si tu inabadilisha ile iliyopo ambayo ilichapishwa kwa mara ya kwanza katika karne ya 19 ila pia itatumia fursa ya teknolojia na kuifanya kupatikana katika mtandao wa Intanet na kuwa rahisi kutumika na watu wengi. Atlas hii pia hutumika kama kitini cha mafunzo ya Wataalamu wa taaluma ya hali ya hewa, Makampuni na katika sekta kama vile huduma za usafiri wa anga na baharini au katika maziwa. Atlasi hii pia itasaidia katika kuleta uelewa mzuri wa matukio ya hali ya hewa ya muda mfupi na mrefu na hivyo kuchangia katika kuokoa maisha ya watu na mali zao, na zaidi sana kuisaidia jamii katika kukabiliana na matukio ya hali ya hewa yaliyo juu au chini sana ya wastani.

Kama tunavyoelewa kuwa hali ya hewa haitambui mipaka kati ya nchi, hivyo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano itaendelea kuiwezesha TMA kusimamia mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa za hali ya hewa ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kwani taarifa hizi ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Kumekuwa na mafanikio mengi makubwa kupitia ushirikiano wa kimataifa chini ya WMO na wadau wengine. Sawia, ubora wa huduma za hali ya hewa zitolewazo na TMA umeendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa licha ya changamoto mbalimbali. Serikali itaendelea kushirikiana na WMO na kuiwezesha TMA kuendelea kutoa huduma bora zaidi zinazokidhi mahitaji ya wadau wote ikiwa ni pamoja na Watumiaji wa bahari, huduma za usafiri wa anga, kilimo, shughuli za ujenzi, afya, nishati n.k. ili kuendelea kulinda maisha ya watu na mali zao, na vilevile kusaidia kutoa maamuzi katika ngazi mbalimbali za maendeleo nchini.

Serikali inaelewa umuhimu wa mifumo ya upimaji wa hali ya hewa kuanzia ngazi za kitaifa hadi kimataifa, umuhimu wa kufanya tafiti zinazohusiana na hali ya hewa, uwepo wa sera na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya masuala ya hali ya hewa. Jamii inahitaji kujengewa uwezo wa kuelewa taarifa za hali ya hewa, kuzifanyia kazi katika kutoa maamuzi yatakayoleta faida na hatimaye kuboresha huduma za hali ya hewa vilevile kutoa mrejesho kwa Wataalamu ambao utasaidia kuboresha zaidi huduma za hali ya hewa kote nchini. Taarifa hizi za hali ya hewa ni vema zikafungashwa katika mfumo utakaoeleweka na jamii kwa urahisi, kupatikana kwa wote na hasa kwa jamii iliyopo

katika mazingira magumu na hatarishi. Hii itasaidia kuratibu na kukabiliana vema na athari za majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa.

Tunapoadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani, Serikali inaelewa jukumu la Mamlaka ya Hali ya Hewa katika kuihusisha jamii na kutoa elimu katika kuelewa matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa kwa lengo hasa la kuongeza uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa nchini. Kaulimbiu ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani mwaka huu "Uelewa wa mawingu na umuhimu wake" ni muafaka kwa wakati huu ambapo jamii na nchi yetu inafanya juhudi kubwa ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa. Malengo haya ni pamoja na kufanya maamuzi yanayozingatia matumizi ya huduma za hali ya hewa, kukabiliana na janga la njaa, maisha ya viumbe hai katika nchi kavu, maisha ya viumbe hai katika maji, upatikanaji wa maji safi na salama, usafi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa kukabiliana na majanga ya asili kama vile ukame na mafuriko.

Serikali itaendelea kuiwezesha TMA katika kuanzisha vituo vipya vya hali ya hewa ambavyo ni muhimu sana katika upimaji wa hali ya hewa kitaifa na kimataifa yaani “Global Climate Observing System (GCOS)”, sambamba na kufanikisha programu ya WMO ya kuunganisha mifumo ya upimaji wa hali ya hewa kote duniani yaani “WMO Integrated Global Observing System (WIGOS)”. Kupitia mipango na miradi ya kitaifa ya maendeleo, Serikali imepanua wigo wa upimaji wa hali ya hewa

kwa kutumia Rada za hali ya hewa na vituo vinavyojiendesha vyenyewe (Automatic Weather Stations) na hivyo kuboresha uwezo wa TMA katika utoaji wa huduma za hali ya hewa. Aidha, upanuzi wa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa bahari na maziwa makuu pamoja na kuendelea kupata cheti cha ubora wa kimataifa cha utoaji wa huduma yaani (ISO Certificate on Quality Management System) katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa anga ni mafanikio muhimu ya kujivunia hasa ikizingatiwa kwamba nchi yetu ilikuwa ya kwanza kwa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara kufikia viwango hivyo mwaka 2011.

Mipango ya Serikali kama hii ina faida kubwa ambazo zinanufaisha sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii na hatimaye kufikia malengo ya Taifa ya ukuaji wa uchumi. Mifano iliyo dhahiri ni pamoja na kuongezeka kwa ubora wa utabiri wa hali ya hewa, kuongezeka kwa tija katika kilimo na usalama wa chakula, usimamizi mzuri wa rasilimali za maji, nishati, kupungua kwa athari zitokanazo na maafa, huduma bora za afya, usafiri, utalii, ujenzi, na mengine mengi ambayo ni muhimu katika kuchangia azma ya nchi ya kufikia Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Jamii .

Katika kuadhimisha siku hii, Serikali inatambua mchango kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wale wa Kimataifa na Kitaifa, Taasisi zisizo za Kiserikali, Taasisi za Sayansi na Utafiti, Shule, Taasisi za Kidini, Watu binafsi, na Umma kwa

ujumla katika kusaidia na kushirikiana na Serikali katika utoaji wa huduma bora za hali ya hewa na kusaidia katika usalama wa maisha ya watu na mali zao. Ni kwa njia hii kwamba afya na maendeleo ya kiuchumi ya watu wetu na wengine yanaweza kufikiwa kwa uhakika zaidi. Hivyo naendelea kuwasihi wadau wote waendelee kushirikiana na Serikali na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua jukumu lake katika kuwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kuhakikisha uwepo wa miundombinu muhimu na upatikanaji wa huduma bora za hali ya hewa kwa jamii na zinazotolewa kwa wakati kwa manufaa ya wananchi wakati wowote zinapohitajika. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma za hali ya hewa zinaendelea kutolewa kwa ufanisi na kwa gharama nafuu na hatimaye kuchangia katika ajenda ya maendeleo ya taifa. Ni matumaini yangu kwamba watendaji wa Serikali kuu na Serikali za Mitaa, wasomi, sekta binafsi, vyombo vya habari na umma wote wataendelea kuunga mkono juhudi na mchango muhimu wa TMA na WMO katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa jamii yetu.

Sambamba na kaulimbiu ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani ya mwaka huu napenda kuhamasisha kila mmoja wetu na umma kwa ujumla kuendelea kutumia taarifa za hali ya hewa kwa ustawi wetu wenyewe na kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi yetu. Ninaamini kwamba huduma zitolewazo na Mamlaka

ya Hali ya Hewa zitaendelea kuwa na umuhimu mkubwa zaidi katika jamii yote nchini na kwa miaka mingi ijayo. Sambamba na hili, Serikali itaendelea kuhakikisha mgawanyo wenye uwiano wa rasilimali muhimu kwa ajili ya utafiti, miundombinu bora na ya kisasa ili kusaidia utoaji huduma bora zaidi za utabiri wa hali ya hewa, ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mwisho, nawatakia wananchi wote wa Tanzania na wadau wa huduma za hali ya hewa duniani kote maadhimisho mema na yenye mafanikio ya siku ya Hali ya Hewa Duniani “Tuyaelewe Mawingu na umuhimu wake”